SHUGHULI ZA KISWAHILI - KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA - CBC GRADE 2 TERM 3 EXAMS 2023

KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA (Alama 5)

Nitakusomea hadithi kisha utajibu maswali nitakayokuuliza.

Sungura mjanja alimtembelea binamu yake mjini. Alipofika kwake, aliviona vyumba vingi. Alijisemea, kila siku nitalala chumba tofauti nihisi jinsi kilivyo.

a. Sungura alimtembelea nani? _____
b. Binamu yake aliishi wapi?
   _____
c. Taja vyumba vitatu vinavyopatikana kwa nyumba.
   _____
   _____
   _____

KUSOMA KWA SAUTI (Alama 10)

Soma hadithi hii kwa sauti. Mwanafunzi asome maneno 40 kwa dakika moja.

Fisi alikuwa amelala siku nyingi. Aliogopa kufa kwa sababu ya njaa. Siku moja kabla ya kwenda mawindoni, alimwomba Mungu amsaidie apate chakula. Akatoka nyumbani kwake akiwa mchovu sana. Ghafla, alimpata ndama amefungwa kwenye mti kwa kamba. Nani kama mimi? Akaanza kujigamba. Alijisifu kuwa yeye ni hodari na siku hiyo haingepita bila yeye kupata mlo.

Mwanafunzi asome maneno 40 kwa dakika moja.